KPC

# SHIRIKA LA BOMBA LA KENYA

# HATI YA HUDUMA KWA WANANCHI

F

Hati Ya Huduma Kwa Wananchi ........ 1
**1.1 Sisi ni nani** ........ 3
**1.2 Mtandao wetu wa bomba** ........ 3
**1.3 Maono yetu** ........ 3
**1.4 Ujumbe wetu** ........ 3
**1.5 Maadili yetu** ........ 3
**1.6 Wito wetu** ........ 3
**2.0 Hati Ya Huduma** ........ 3
**2.1 Huduma zetu** ........ 4
**2.2 Wateja wetu** ........ 4
**2.3 Kanuni zetu za huduma za uendeshaji** ........ 4
**2.4 Viwango vya huduma zetu** ........ 5
**2.5 Kujitolea kwa wadau wetu** ........ 5
**2.6 Haki Zako** ........ 5
**2.7 Masaa yetu ya ofisi** ........ 6
**3.0 Mawasiliano Yetu** ........ 7
**4.0 Hati Ya Huduma Ya Shirika La Bomba La Kenya (KPC)** ........ 9

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Sisi ni nani

Kampuni ya Kenya ya bomba (KPC) ni shirika linalomilikiwa na serikali ya Kenya chini ya wizara ya nishati na madini kitengo cha petroli iliyoingizwa mwaka wa 1973 chini ya sheria ya makampuni ya (kifungu) 486, Shughuli zetu za biashara zilianza mwaka wa 1978 na mamlaka ya misingi ya kusafirisha, kuhifadhi na kutoa bidhaa za petroli kwa usalama na ufanisi kutoka Mombasa hadi mikoani na nchi jirani kupitia mtandao wa bomba.

### 1.2 Mtandao wetu wa bomba

Mtandao wa bomba sasa unajumuisha Kilomita 450 ya msitari wa -1 kutoka bandari ya Mombasa hadi Nairobi, kilomita 325 ya msitari wa -2 na 4 kutoka Nairobi hadi Eldoret na kilomita 121 ya msitari wa -3 na 6 kutoka Sinendet hadi Kisumu na jumla kilomita 1,792.

### 1.3 Maono yetu

Kampuni bora Zaidi ya mafuta na gesi Afrika.

### 1.4 Ujumbe wetu

'Kubadili Maisha kupitia utoaji wa mafuta na gesi bora kutoka kwa chanzo hadi kwa wateja'

### 1.5 Maadili yetu

Maadili yetu saba yatakuwa msingi wa utamaduni wa ushirika ambao unamalengo ya kujenga utendaji kazi wa kiwango cha juu:

- Uadilifu;
- Uwazi;
- Uajibikaji;
- Moyo wa kundi;
- Bidii;
- Uaminifu na
- Utunzaji wa mazingira.

### 1.6 Wito wetu

Wito wetu wa kuunganisha kufanya vizuri Zaidi utawahimiza wafanya kazi wote kuimarisha utendaji kazi wa mtu binafsi na kwa pamoja ili kuwezesha utoaji wa maono ya mwaka 2025.

## 2.0 HATI YA HUDUMA

Hati ya huduma ni uonyesho wa kujitolea kwetu katika kuboresha huduma zetu na kuzungumzia nyinyi wadau wetu.

Ni taarifa ya nia kwa wateja wetu, wadau na umma (wananchi) ambayo inasema sisi ni nani, mamlaka yetu na huduma tunazotoa.

Pia inajumuisha viwango vinavyotarajiwa kwetu na jinsi wadau wetu wanavyoweza kutafuta kurekebisha ikiwa hawajathamini huduma zetu.

Mkataba huu utatuongoza katika utuoji wa huduma zetu kuhakikisha majibu kwa wakati na hivyo kusaidia kuboresha utoaji wa huduma

## 2.1 Huduma zetu

Tunatoa huduma sifuatazo:

1. Kupokea na kurudi kupakia bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa kutoka na kuingia kwenye meli
2. Usafiri, kuhifadhi na kugawa bidhaa zifuatazo za mafuta ya petrol:
   - Petroli ya magari bila madini ya risasi (Daraja bora)
   - Petroli ya magari bila madini ya risasi (Daraja la kawaida)
   - Magari gesi mafuta (dizeli)
   - Mafuta ya taa
   - Mafuta ya ndege
3. Huduma za kupima mahabara kwa vyeti bora vya bidhaa ya petrol
4. Upangishaji wa kebo ya nyuzinyuzi (FOC) ya KPC.
5. Taasisi ya Mafuta na Gesi ya Morendat (MIOG) mjini Mombasa, Nairobi, Naivasha na Eldoret

## 2.2 Wateja wetu

Wao ni pamoja na:

1. Makampuni ya masoko ya mafuta
2. Serikali ya Kenya
3. Wauzaji wa bidhaa na huduma
4. Waajiriwa na
5. Umma kwa jumla

## 2.3 Kanuni zetu za huduma za uendeshaji

Kupitia mkataba huu tunajiweka kwa:

i. Kushika na kukuza viwango vya juu vya taaluma
ii. Kukuza matumizi ya ufanisi na kiuchumi wa rasirmali
iii. Kutoa huduma nzuri, zilizo sawa na haki na za usawa
iv. Kuwa msikivu kwa mahitaji ya wadau wetu
v. Kuwa na uwazi na uajibikaji katika utoaji wetu wa huduma
vi. Kushikamana na utawala bora wa ushirika
vii. Kushughulikia wadau wetu kwa heshima, hisani na heshima kubwa

viii. Kutibu habari zinazotolewa na wadau wetu kwa uadilifu
ix. Kukuza nguvu na mazoea ya ubunifu kupitia maboresho ya kuendelea na mifumo
x. Kutoa kwa jamii kwa kushiriki katika mipango ya shirika kwa wajibu wa jamii

## 2.4 Viwango vya huduma zetu

Tumejitolea kwa:

i. Jibu simu zote haraka na kwa heshima; ndani ya sekunde kumi na tano.
ii. Kukaribisha na kuhudumia wageni wote punde tu wanapofika na kwa heshima ndani ya dakika moja.
iii. Tambua haraka barua zote; barua za ndani ndani ya saa arobaini na nane na za nje ndani ya siku tano za kazi;
iv. Kufuata taratibu zetu za ndani na za uendeshaji huduma;
v. Kufuata kanuni zote za serikali, sheria na viwango vya kimataifa vinavyotuhusu.

Viwango hivi vya juu kati ya vingine vinaendelea kupitiwa mara kwa mara ili kuboresha utoaji wa huduma zetu.

## 2.5 Kujitolea kwa wadau wetu

Kwa kutambua matarajio ya wadau wetu tunajitolea:

i. Kutoa huduma kwa kitaalamu;
ii. Kuletea bidhaa na huduma zilizothibitishwa na ubora;
iii. Kuwa na heshima na kusaidia;
iv. Kufanya mambo sahihi mara ya kwanza;
v. Kutoa taarifa sahihi na sawa;
vi. Kuwa na uwajibikaji na uwazi;
vii. Kutoa usalama na ulizi ndani ya mfumo;
viii. Kutoa huduma za gharama nafuu na kwa wakati unaofaa;
ix. Kukumbatia mawazo mapya, ubunifu na teknolojia zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma;
x. Kutunza taarifa za siri zilizotolewa na wadau wetu;
xi. Kudumisha uadilifu na uaminifu katika utoaji wa huduma zetu;
xii. Kuzingatia sheria za ardhi na majukumu ya kisheria na kuhakikisha Shughuli zetu zinahifadhi mazingira

## 2.6 Haki Zako

Una haki ya:-

i. Kuuliza au kulalamika kama hujaridhishwa na kiwango cha huduma zilizotolewa
ii. Elekeza mwaswala yoyote yanayohusiana na huduma kwa afisi ya juu.
iii. Toa mapendekezo ambayo yanaweza kuwezesha shirika kutoa huduma bora.
iv. Hisani na ustahili katika Shughuli zako na sisi.
v. Huduma bora bila kutoa rushwa.

vi. Maoni/majibu kwa maswala yanayokuathiri wewe.
vii. Kushughulikia malalamishi.
viii. Malalamishi kutoka kwa wateja wasioridhika yatashughulikiwa haraka papo hapo wakati wa huduma.

## 2.7 Masaa yetu ya ofisi

Bomba hufanya kazi saa 24, kwa siku 365/366 kwa mwaka.
Masaa ya ofisi ni Jumatatu hadi Ijumaa
Saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni



KPC - Public

## 0 MAWASILIANO YETU

| | |
|---|---|
| **1. Makao Makuu,**<br>Kenpipe Plaza, Barabara ya Sekondi, nje ya barabara ya Nanyuki, Eneo la viwandani<br>S. L. P. 73442 – 00200, Nairobi.<br>Simu: +254 020 2606500/1/2/3/4<br>+ 254 709 723 000<br>Tovuti: kpc.co.ke<br>Barua pepe: complaints@kpc.co.ke; customerservice@kpc.co.ke; info@kpc.co.ke | **2. Kituo cha Pampu nambari 1 (Changamwe)**<br>Bararara ya zamani ya Magongo,<br>S. L P 93231-80100, Mombasa.<br>Simu: +254 722 207670<br>Barua pepe: msa@kpc.co.ke |
| **3. Kituo cha Pampu nambari 2 (Samburu)**<br>S. L. P. 93231-80102, Mombasa.<br>Simu: +254 775 251141<br>Barua pepe : samburu@kpc.co.ke | **4. Kituo cha Pampu nambari 3 (Maungu)**<br>S. L. P. 119 – 80300, Voi.<br>Simu: +254 713 837091<br>Barua pepe : maungu@kpc.co.ke |
| **5. Kituo cha Pampu nambari 4 (Manyani)**<br>S. L. P. 119-80300, Voi.<br>Simu: +254 719 124046 | **6. Kituo cha Pampu nambari 5 (Mtito Andei)**<br>S. L. P. 41-90128, Mtito Andei |
| **7. Kituo cha Pampu nambari 6 (Makindu)**<br>S. L. P. 108 Makindu<br>Simu: +254 739 906 613<br>Barua pepe: makindu@kpc.co.ke | **8. Kituo cha Pampu nambari 7 (Sultan Hamud)**<br>S. L. P. 93231 – 90132 Sultan Hamud<br>Simu: +254 736 729374<br>Barua pepe : sultan@kpc.co.ke |
| **9. Kituo cha Pampu nambari 8 (Konza)**<br>Simu: 3936672<br>Barua pepe : konza@kpc.co.ke | **10.Kituo cha Pampu nambari 9 (Embakasi)**<br>Embakasi Aviation Depot, Outering Rd,<br>S. L. P. 73442 – 00200, Nairobi.<br>Simu: +254 722 207677<br>Barua pepe: embakasi@kpc.co.ke |



KPC - Public

| | |
|---|---|
| **11.Kituo cha Pampu nambari 10, (Eneo la viwandani)**<br>Nairobi Terminal, Barabara ya Sekondi, nje ya barabara ya Nanyuki,<br><br>S. L. P. 73442 – 00200, Nairobi<br>Simu: +254 722 207678/<br>+254 722 207679<br>Barua pepe: info@kpc.co.ke | **12.Kituo cha Pampu nambari 12 (Moi Airport)**<br>S. L. P. 93231 – 80102, Mombasa.<br>Simu: 254 725 702067<br>Barua pepe: moiairport@kpc.co.ke |
| **13.Kituo cha Pampu nambari 14 (Kipevu)**<br>S. L. P. 93231 0 80100, Mombasa.<br>Simu: +254 724 146164<br>Barua pepe: kipevu@kpc.co.ke | **14.Kituo cha Pampu nambari 22 (Ngema)**<br>S. L. P. 73442 – 00200, Nairobi.<br>Simu: +254 50 50525<br>Barua pepe: ngema@kpc.co.ke |
| **15.Kituo cha Pampu nambari.23 (Morendat)**<br>S. L. P. 355 – 20117,Naivasha<br>Simu: 0726738968<br>Barua pepe: morendat@kpc.co.ke | **16.Kituo cha Pampu nambari 24 (Soilo)**<br>S. L. P. 9722 – 20100, Nakuru<br>Simu: +254 51 214866<br>Barua pepe: nku@kpc.co.ke |
| **17.Kituo cha Pampu nambari 25 (Lanet)**<br>S. L. P. 7722 – 20100, Nakuru<br>Simu: 254 722 207676<br>Barua pepe: nku@kpc.co.ke | **18.Kituo cha Pampu nambari.27 (Eldoret)**<br>Eldoret Depot,<br>S. L. P. 4338- 30100 , Eldoret<br>Simu:254 722 207674<br>Barua pepe: eld@kpc.co.ke |
| **19.Pump Station No.28 (Kisumu)**<br>P.O. Box 609 – 40100 Kisumu.<br>Tel: 254 722 207673<br>Email: ksm@kpc.co.ke | **20.Chuo cha Mafunzo na Mkutano cha Morendat,**<br>S. L. P. 355-20117, Naivasha.<br>Simu: 254 726 738 968<br>Barua pepe: Morendat@kpc.co.ke |

## 4.0 HATI YA HUDUMA YA SHIRIKA LA BOMBA LA KENYA (KPC)

EPUBLIC OF KENYA

**SHIRIKA LA BOMBA LA KENYA (KPC)**

**HATI YA HUDUMA KWA WANANCHI**

| | Huduma/Bidhaa | Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa | Gharama ya Huduma/Bidhaa | Muda bora |
|---|---|---|---|---|
| . | Majibu kwa simu | Simu kutoka kwa mteja | Bila malipo | Sekunde 15 |
| . | Majibu kwa maswali ya wateja | Tembelea ofisi zetu | Bila malipo | Dakika 1 |
| . | Majibu kwa Barua | Andika barua | Bila malipo | Siku 5 za kazi |
| | | Barua pepe na Mitandao ya kijamii (Twitter/X, Facebook na You Tube) | Bila malipo | Siku 1 ya kazi |
| . | Majibu kwa malalamiko ya umma | Lalamika | Bila malipo | Siku 1 ya kazi |
| . | Utatuzi wa malalamiko | Ripoti au andika barua ya malalamiko | Bila malipo | Siku 14 za kazi |
| . | Usajili wa wasambazaji | a) Fomu ya maombi iliyojazwa ipasavyo<br>b) Wasifu wa kampuni<br>c) Cheti cha Usajili/Uchanganuzi wa Kampuni<br>d) Cheti cha PIN | Bila malipo | Siku 14 za kazi |

| | Huduma/Bidhaa | Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa | Gharama ya Huduma/Bidhaa | Muda bora |
|---|---|---|---|---|
| | | e) Cheti Halali cha Uzingatiaji Kodi/Kutotoa kodi<br>f) Taarifa Halisi za Benki<br>g) Nakilishi ya cheti cha usajili na mamlaka za udhibiti<br>h) Risiti ya malipo yasiyorejeshewa<br>i) Nakili za fomu za marejesho ya kila mwaka zilizojazwa na rejista ya kampuni<br>j) Kitambulisho cha Taifa/Pasipoti | | |
| **7.** | Usindikaji wa zabuni | Wasilisha zabuni kwa bidhaa na huduma | Bila malipo | Siku 90 |
| **8.** | Taarifa ya washindi na waliopoteza zabuni | Fikia lango la e-ununuzi kwa taarifa | Bila malipo | Siku 1 ya kazi |
| **9.** | Malipo kwa bidhaa na huduma zilizopokelewa | Malipo kwa bidhaa na huduma zilizopokelewa /L.P.O/Ankara ya Malipo Cheti cha Kumaliza/Bidhaa/Huduma Zilizopokelewa | Bila malipo | Siku 60 za kazi kuanzia tarehe ya kupokea muswada |
| **10.** | Utupaji wa bidhaa za zamani | Uwasilishaji wa zabuni | Bila malipo | Siku 60 kutoka tarehe ya tangazo |
| **11.** | Ushiriki wa umma katika mchakato wa kutengeneza sera | Kujua masuala na kushiriki | Bila malipo | Siku 1 |
| **12.** | Uajiri wa wafanyakazi | Fanya maombi rasmi kulingana na tangazo | Bila malipo | Siku 90 |
| **13.** | Uchambuzi wa ombi la taarifa | Tuma ombi la taarifa | Bila malipo | Siku 21 |

| | Huduma/Bidhaa | Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa | Gharama ya Huduma/Bidhaa | Muda bora |
|---|---|---|---|---|
| **14.** | Mkataba wa usafirishaji na uhifadhi wa usafirishaji wa bomba, uhifadhi na usambazaji wa bidhaa za petroli zilizosafishwa. | a) Barua ya maombi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika La Bomba la Kenya<br>b) Utoaji wa hati za; mahitaji ya leseni na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Petroli (EPRA), usajili wa Wizara ya Nishati na Petroli (MOEP), Mamlaka ya Mapato ya Kenya (KRA)<br>c) Ukaguzi unaostahili<br>d) Utoaji wa kima cha chini cha kujaza laini 1,000 mita za ujazo.<br>e) Mkataba wa Usafirishaji na Uhifadhi uliosainiwa (TSA) | Bila malipo | Miezi sita |
| **15.** | Kusukuma mafuta katika Kituo cha Nairobi na Kituo cha Mafuta cha Shimanzi (SOT) Mombasa | a) Uthibitisho wa kuwepo kwa raslimali ya mafuta kupitia kwa mfumo wa lango la mteja wa KPC.<br>b) Ombi la kusukuma mafuta kutoka kwa Kampuni ya Uuzaji wa Mafuta<br>c) Taarifa ya Nia (NOI)<br>d) Notisi ya siku 14 kwa matumizi ya tawi la bomba<br>e) Kuzingatia marshati ya Mkataba wa usafirishaji na uhifadhi uliosainiwa | **Shilingi za Kenya /mita za ujazo**<br>**2023/24** - 2,582.72<br>**2024/25** - 2,791.85 | Kulingana na tasnia iliyokubaliwa ya muda wa uhamisho wa mafuta. |
| **16.** | Uagizaji, ada ya utunzaji na uhifadhi msingi wa mafuta katika KOSF na Kenya Petroleum Refineries Limited (KPRL) | a) Cheti cha Ubora wa Usafishaji<br>b) Cheti cha kuachiliwa kutoka Bandari ya Kupakia | **Dola za Marekani/mita za ujazo, bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT).**<br>a) Ada ya Utunzaji - 0.19<br>b) Ada ya uhifadhi msingi- 3.55 | Kwa mujibu wa ratiba ya meli, Muda wa kuhifadhi |



KPC - Public

<table>
<tr><th></th><th>Huduma/Bidhaa</th><th>Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa</th><th>Gharama ya Huduma/Bidhaa</th><th>Muda bora</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td>c) Karatasi ya Ulinganisho na Uthibitishaji upya wa idadi iliyopakiwa ya Meli dhidi ya tanki inayotoa<br>d) Stakabadhi ya shehena kutoka Bandari iliyopakia<br>e) Ripoti ya Mkaguzi/Wakadiriaji wa mizigo iliyotangulia<br>f) Historia ya safari kutoka kwa meli /Nahodha wa meli<br>g) Barua ya malalamishi kutoka Bandari ilipopakia, inapohitajika<br>h) Ripoti ya nafasi ya kupokea bidhaa<br>i) Hesabu ya Sampuli<br>j) Karatasi ya Data ya Usalama wa Nyenzo<br>k) Cheti cha Kutolewa kwa Wingi cha Shirika la Viwango la Kenya (KEBS).<br>l) Mkataba wa Usafirishaji na Uhifadhi uliosainiwa (TSA)</td><td></td><td>kulingana na Mkataba wa Usafirishaji na Uhifadhi uliosainiwa</td></tr>
<tr><td>17.</td><td>Upakiaji wa lori Petrocity (Konza), Nakuru, Eldoret, Kisumu, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Moi (MIA) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA)</td><td>a) Hati za utambulisho za lango la mfumo wa KPC.<br>b) Utoaji wa hati za sampuli za agizo<br>c) Cheti cha uzingatiaji cha EPRA<br>d) Bima halali ya lori na nyaraka za urekebishaji.<br>e) Leseni halali ya dereva</td><td>* Ushuru wa Ndani: Shilingi za Kenya /mita za ujazo, pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)
<table>
<tr><th>Huduma</th><th>2023/24</th><th>2024/25</th></tr>
<tr><td>Petrocity (Konza)</td><td>1,420.73</td><td>1,527.48</td></tr>
<tr><td>Nakuru</td><td>3,211.26</td><td>3,467.62</td></tr>
<tr><td>Eldoret</td><td>3,869.56</td><td>4,175.37</td></tr>
<tr><td>Kisumu</td><td>3,865.84</td><td>4,171.37</td></tr>
</table></td><td>Upakiaji wa lori<br>Ndani ya nchi- Masaa 1- 3<br>Nje ya nchi- Masaa 1-4</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th></th><th>Huduma/Bidhaa</th><th>Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa</th><th>Gharama ya Huduma/Bidhaa</th><th>Muda bora</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td>f) Idhini kutoka kwa EPRA ya upakiaji wa mafuta ya ndege/mafuta taa.<br>g) Kuzingatia marshati ya Mkataba wa usafirishaji na uhifadhi uliosainiwa</td><td>*Ushuru wa kuuza nje: (Dola za Marekani /mita za ujazo bila VAT)<table><tr><th>Huduma</th><th>2023/24</th><th>2024/25</th></tr><tr><td>Nakuru</td><td>29.09</td><td>31.42</td></tr><tr><td>Eldoret</td><td>35.06</td><td>37.83</td></tr><tr><td>Kisumu</td><td>35.02</td><td>37.79</td></tr></table></td><td>Upakiaji wa mafuta ya ndege (JetA-1)<br>Ndani ya nchi: Saa 1<br>Nje ya nchi: Saa 1</td></tr>
<tr><td>18.</td><td>Huduma za bomba la anga katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Moi (MIA) na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA)</td><td>a) Hati za thibitisho za agizo la kupakia.<br>b) Uthibitisho wa wa kuwepo kwa raslimali ya mafuta kupitia mfumo wa lango la mteja wa KPC.<br>c) Chati halali cha urekebishaji wa mita ya kusambaza mafuta.<br>d) Kuzingatia marshati ya Mkataba wa usafirishaji na uhifadhi uliosainiwa</td><td>Dola za Marekani /mita za ujazo, ( bila VAT)<table><tr><th>Huduma</th><th>2023/24</th><th>2024/25</th></tr><tr><td>MIA</td><td>23.40</td><td>25.29</td></tr><tr><td>JKIA</td><td>23.40</td><td>25.29</td></tr></table></td><td>Masaa 24 kulingana na mahitaji ya ndege</td></tr>
</table>



KPC - Public

| | Huduma/Bidhaa | Mahitaji ya kupata Huduma/Bidhaa | Gharama ya Huduma/Bidhaa | Muda bora |
|---|---|---|---|---|
| **19.** | Upangishaji wa kebo ya nyuzinyuzi (FOC) ya KPC. | a) Barua ya maombi<br>b) Leseni ya Halmashauri ya Mawasiliano ya Kenya<br>c) Uidhinishaji wa aina ya vifaa kutoka kwa Halmashauri ya Mawasiliano ya Kenya<br>d) Cheti cha Kusajiliwa<br>e) Hati ya Muungano<br>f) Kifungu cha Muungano<br>g) Cheti cha nambari ya siri<br>h) Cheti cha VAT<br>i) Cheti cha Kuzingatia Ushuru<br>j) Taarifa za fedha za miaka 3<br>g) Fomu ya kujiandikisha(CR12) | a) Upangishaji wa kebo ya nyuzinyuzi -Dola za Marekani 22/nyuzi/kilomita<br>b) Ada ya Matunzo - 5% ya jumla ya kiwango cha kupangisha<br>c) Usakinishaji –Dola za Marekani 200 kwa kila eneo (Malipo ya mara moja).<br>d) Mahali pamoja; malipo ya mara moja ya usakinishaji ya Dola za Marekani 3,900 kwa kila kabati na ada ya Dola za Marekani 850 kwa kabati kwa mwaka. | Siku 30 - 60 |

***Sheria na Masharti Kutumika.**

*Shughuli zote za biashara kwa bidhaa za mafuta ya petroli na gesi ya kupikia (LPG) ni kwa mujibu wa Makubaliano ya Usafirishaji na Uhifadhi (TSA) iliyotiwa saini.

*Bidhaa na huduma zote za ndani zinajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ilhali huduma za mauzo ya nje hazijumuishi VAT.

* Ushuru wa bidhaa za mafuta huwekwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Petroli (EPRA), sambamba na TSA na hutegemea uhakiki wa mara kwa mara.

Hati ya utoaji huduma ya Mwananchi inapatikana kwenye tovuti yetu: www.kpc.co.ke

**HAKIKISHO;**
Tumejitolea kwa ungwana na ubora katika utoaji wa huduma.

Huduma/bidhaa yoyote inayotolewa ambayo haiambatani na viwango vilivyo ratibishwa hapo juu au afisa yeyote ambaye haafikii ahadi ya uungwana na ubora katika Utoaji Huduma inapaswa kuripotiwa kwa:

| 1. Mkurugenzi Mkuu, | 2. Katibu wa Tume/Afisa Mtendaji Mkuu, |
| --- | --- |
| Shirika la Bomba la Kenya,<br>Ghorofa ya 6, Kenpipe Plaza,<br>Barabara ya Sekondi nje ya Barabara ya Nanyuki, Eneo la Viwandani,<br>S.L.P 73442-00200 Nairobi, Kenya.<br>Simu : +254 020 2606500/1/2/3/4<br>Simu ya rununu: +254 709 723 000<br>Tovuti: www.kpc.co.ke<br>Barua pepe: complaints@kpc.co.ke; customerservice@kpc.co.ke au info@kpc.co.ke | Tume ya Haki ya Utawala,<br>Ghorofa ya 2, West End Towers,<br>Barabara ya Waiyaki , Nairobi.<br>S.L.P 20414-00200 Nairobi<br>Simu: +254 (0)20 2270000/0800 221 349 (Nambari isiyolipiwa)<br>Barua pepe: info@ombudsman.go.ke;<br>complain@ombudsman.go.ke |
| ***HUDUMA BORA NI HAKI YAKO*** | |

**SAHIHI:**............................................................................ **TAREHE:** 11-07-2025 ........................................

**MKURUGENZI MKUU**